



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA ITILIMA



Unapojibu taafadhali taja:

Kumb. Na.AN.191/226/03 'A'/4.

Tarehe :06/08/2020

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Itilima anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi ya **Mtendaji wa Kijiji III**. Tangazo hili limetokana na Kibali cha Ajira Mbadala chenye Kumb.Na. FA.17/533/01/"A"/122 cha tarehe 30/06/2020 kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

1 MTENDAJI WA KIJIKI III – NAFASI 1

1.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Awe amehitimu wa Kidato cha IV au VI aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika mojawapo wa fani zifuatazo: **Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Jamii** kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

1.2 MAJUKUMU

- i. Afisa Masuuli (Mhasibu) na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
- ii. Kusimamia ulinzi na Usalama wa raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika kijiji.
- iii. Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya kijiji.
- iv. Katibu wa mikutano na kamati zote za Halmashauri ya kijiji.
- v. Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
- vi. Kuandaa Taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
- vii. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalum katika Kijiji.
- viii. Kusimamia ukusanyaji na kuhifadhi kumbukumbu zote za nyaraka za Kijiji.
- ix. Mwenyekiti wa kikao cha Wataalamu waliopo katika Kijiji.
- x. Kupokea, Kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi.
- xi. Kusimamia utungaji wa sheria Ndogo za Kijiji na

Halmashauri ya Wilaya ya Itilima, S. L. P 308, Itilima, Simu +255 028 2986329, Barua pepe: info@itilimadc.go.tz.

Tovuti: www.itilimadc.go.tz

xii. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

1.3 MSHAHARA

Kwa kuzingatia Ngazi za Mishahara ya Serikali TGS.B

2 MASHARTI YA JUMLA

- i. Waombaji wote wawe ni raia wa Tanzania wenye umri kati ya miaka 18 hadi 45.
- ii. Muombaji awasilishe picha moja ya hivi karibuni.
- iii. Waombaji wawasilishe Maelezo binafsi yanayojitosheliza (Detailed CV) yenye anuani na namba za simu pamoja na majina ya wadhamini watatu (Referees) na namba zao za simu.
- iv. Waombaji wote waambatanishe nakala ya vyeti halisi vya masomo na taaluma (NTA level 5) transcript ya cheti cha taaluma na cheti cha kuzaliwa. Muombaji atakayewasilisha "Result slip", "statement of results", "Provisional results" au "Transcript" bila nakala halisi ya cheti cha taaluma maombi yake hayatakubaliwa.
- v. Kwa waliosoma nje ya nchi elimu ya kidato cha nne na kidato cha sita wawasilishe uthibitisho kutoka Baraza la Mitahani la Tanzania (NECTA).
- vi. Kwa waliomaliza vyuo nje ya nchi wawasilishe uthibitisho kutoka Baraza la Elimu ya Ufundi la Taifa (NACTE).
- vii. Wote watakaokidhi vigezo ndio watakaoitwa kwenye usaili (Interview).
- viii. Maombi yasiyozingatia vigezo vilivyoinishwa hayatashughulikiwa.
- ix. Mwisho wa kupokea maombi haya ni tarehe 19/08/2020 saa 9:30 Alasiri.

MUHIMU: Kumbuka kuambatanisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vielelezo vyote vilivyohitajika. Maombi yote yatumwe Kwa:-

MKURUGENZI MTENDAJI,

HALMASHAURI YA WILAYA,

S.L.P . 308

ITILIMA.

Tangazo hili pia linapatikana kwenye Tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Itilima
www.itilimadc.go.tz



Elizabeth M Gumbo

Mkurugenzi Mtendaji

Halmashauri ya Wilaya ya Itilima

**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
ITILIMA**

Halmashauri ya Wilaya ya Itilima, S. L. P 308, Itilima, Simu +255 028 2986329, Barua pepe: info@itilimadc.go.tz.

Tovuti: www.itilimadc.go.tz